

Please check the examination details below before entering your candidate information

Candidate surname

Other names

Centre Number

Candidate Number

| | | | | |
|--|--|--|--|--|
| | | | | |
|--|--|--|--|--|

| | | | | |
|--|--|--|--|--|
| | | | | |
|--|--|--|--|--|

Pearson Edexcel International GCSE

Time 2 hours 15 minutes

Paper
reference

4SW1/01

Swahili

PAPER 1: Reading, Writing and Translation



You do not need any other materials.

Total Marks

Instructions

- Use **black** ink or ball-point pen.
- **Fill in the boxes** at the top of this page with your name, centre number and candidate number.
- There are **three** sections you must answer:
 - Section A Questions 1–4
 - Section B Questions 5 and either Question 6(a) or 6(b) or 6(c)
 - Section C Question 7.
- Answer the questions in the spaces provided
 - *there may be more space than you need.*
- You must **not** use a dictionary.

Information

- The total mark for this paper is 80.
- The marks for **each** question are shown in brackets
 - *use this as a guide as to how much time to spend on each question.*

Advice

- Read each question carefully before you start to answer it.
- Check your answers if you have time at the end.

Turn over ►

P71077A

©2021 Pearson Education Ltd.

E:1/1/1/1



Pearson

SECTION A**Reading**

Answer ALL questions. Write your answers in the spaces provided.

Some questions must be answered with a cross in a box . If you change your mind about an answer, put a line through the box and then mark your new answer with a cross .

Open-response questions do not have to be written in full sentences and you may respond using single words or phrases.

- 1 Malizia sentensi zifuatazo kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Weka alama sahihi kwenye kila kisanduku.

Sikukuu

Siku hizi, wakati wa sikukuu tofauti, watu hununua zawadi kwa ndugu na marafiki. Maduka hujaribu kuwavutia wateja kwa kutangaza bidhaa zao kwenye magazeti na runinga. Zamani watu walitoa pesa na si zawadi.

Mimi ninapendelea zaidi kununua zawadi. Miezi kadhaa kabla ya sikukuu mimi huenda mjini na huzunguka madukani huku nikitafuta zawadi. Wakati mwingine hununua mitandaoni pia ingawa ninapendelea zaidi kuona ninachokinunua. Mara nyingi hupenda kununua vitabu, michezo tofauti na pia wanasesere.

Mwaka huu nimeamua kujali zaidi kuhusu mabadiliko ya tabia nchi kwa hivyo nitatuma salamu za sikukuu kwa kutumia mitandao. Pia nimeamua kufunga zawadi zangu kwa kutumia magazeti ya zamani yasiyohitajika tena na si mifuko mipya ya karatasi.



- | | | | |
|----------------------|-----------------------------|---------------------------|----------------|
| A madaftari | B sikukuu | C vyombo vyahabari | D miezi |
| E mitandaoni | F sokoni | G mazingira | H miaka |
| I salamu | J magazeti ya zamani | K zawadi | L fedha |
| M mwanasesere | | | |

| Example: | | K |
|-----------------|--|----------|
| 1 (a) | Wakati wa sikukuu watu hutoa... | |
| 1 (b) | Zawadi hutangazwa kwenye... | |
| 1 (c) | Zamani ... ziligawiwa wakati wa sikukuu | |
| 1 (d) | Msako huanza ... michache kabla ya sikukuu | |
| 1 (e) | Zawadi hupatikana madukani na... | |
| 1 (f) | ... ni zawadi nzuri kwa watoto | |
| | ... yatatumiwa kufunga zawadi | |

(Total for Question 1 = 6 marks)



P 7 1 0 7 7 A 0 3 1 6

- 2 Weka alama katika visanduku **10** vilivyo sahihi. Sentensi nyingine au watu wengine wanaweza kuwa na alama zaidi ya moja au bila alama yoyote.

Familia

Miranda



Mimi ninapenda kuwa peke yangu na hivi karibuni nilihamia Nairobi. Nimeweka mapambo machache nyumbani kwangu hivyo panaonekana kama hoteli. Ninadhani ni sawa kutokuwa na pesa ila kuwa na uhuru wangu. Ninamkumbuka sana mama yangu aliyependa kunipikia vyakula vitamu. Simkumbuki kaka yangu aliyependa kufanya utani wa kipuuzi.

Aziza



Nitahama kutoka kwetu na nitaishi kwenye nyumba nzuri iliyopo katikati ya Nairobi. Wazazi wangu wamenisaidia kulipa kodi ya mwezi wa kwanza. Ninapenda kuishi na familia yangu hivyo ninahisi mwanzoni nitarudi nyumbani kila siku ili niweze kula vyakula vya mama.

Kosgei



Hakuna anayeweza kunichekesha kama kaka yangu. Wiki ijayo, nitakapoenda peke yangu kutembea Nairobi, nitamkumbuka sana. Nina hamu ya kuonja vyakula tofauti na vile vya mama yangu nitakapofika huko. Wazazi wangu wameshalipia hoteli.



| | | Miranda | Aziza | Kosgei |
|--------|--------------------------------|-------------------------------------|-------------------------------------|-------------------------------------|
| Mfano: | Wazazi hawapendi kusumbua watu | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> |
| A | Haishi na wazazi hivi sasa | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> |
| B | Anapenda chakula cha mama | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> |
| C | Anapenda kuwa peke yake | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> |
| D | Atafikia nyumba ya wageni | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> |
| E | Kaka anapenda utani unaokera | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> |
| F | Anaishi Nairobi sasa | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> |
| G | Amesaidiwa na wazazi kifedha | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> | <input checked="" type="checkbox"/> |

(Total for Question 2 = 10 marks)

- 3** Soma makala kuhusu Likizo mjini Kilwa. Malizia taarifa kwa kutumia namba au maneno kwa **Kiswahili**.

Likizo mjini Kilwa

Mimi na familia yangu tumekuja Kilwa kupumzika. Ni mji uliopo Kusini mwa Tanzania. Nimefurahia sana kuweza kuzungumza Kiswahili kwani nilijifunza lugha hii muhula uliopita katika chuo kikuu kinachojudikana huko London.

Leo tuna mpango wa kula chakula katika mgahawa uliopo mkabala na bahari. Wazazi wangu wananiegemea ili kuwasiliana na wahudumu wote na pia kuvielewa vyakula vya Kiswahili. Leo itakuwa mara yetu ya kwanza kula samaki, kachumbari na ugali. Baadaye tutaenda kutembelea magofu yaliyo nje ya mji na kujifunza historia ya mji huu. Pia tutaenda sokoni kununua kanga na vinyago. Mimi nisingependa kuenda kote huko, ningefurahia zaidi kuogelea baharini.

Mwaka ujao ninataka kuja Kilwa tena. Nitakuja na rafiki zangu wa shule ili niweze kufurahia mambo yanayonivutia tu. Bila shaka nitawakumbuka wazazi wangu kwani kuwa na familia ni faraja na pia itabidi nijilipie kila kitu mwenyewe.

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



Mfano: Mahali alipotembelea: **Kilwa**

- (a) Mji upo upande wa mwa Tanzania. (1)
- (b) Muda aliojifunza Kiswahili: (1)
- (c) Mgahawa upo karibu na (1)
- (d) Wajibu mgahawani: na (2)
- (e) Habari za kihistoria zinapatikana: (1)
- (f) Sokoni atanunua: na (2)
- (g) Shughuli inayomvutia mwandishi: (1)
- (h) Mwandishi atarudi Kilwa pamoja na: (1)
- (i) Faida za kusafiri na familia ni: na (2)

(Total for Question 3 = 12 marks)



- 4 Soma habari ifuatayo kutoka kitabu kitiwacho **Njama**, kilichoandikwa na A. E. Musiba.

Willy Gamba

Ninaitwa Willy Gamba. Ilikuwa saa tatu kamili niliposimama mbele ya chumba nambari 208 katika ghorofa ya pili ya jumba la kufikia wageni la Kilimanjaro, niligonga mlango mara mbili haraka haraka, halafu nikatulia kidogo kisha nikaupiga mlango teke kidogo. Hivi ndivyo nilivyokuwa nimeelekezwa.

"Karibu", nilimsikia Veronika akijibu. Niliingia na kumkuta amekunja uso huku akiniangalia. Aliponiona hakusubiri kunisalimia bali alitoa sauti kali na kuniarifu kwamba alikuwa London na huko aligundua kwamba mimi, Willy Gamba ni mpelelezi mashuhuri wa Afrika.

Tofauti na nilivyomwambia, aligundua kwamba mimi nimehitimu katika chuo kikuu cha Dar es Salaam na kupata shahada katika sheria. Baada ya masomo nilichaguliwa kwenda kujifunza mambo ya upelelezi nchi mbali mbali kama vile Uingereza, Urusi, na Japan. Kutokana na mafunzo haya ninajulikana kama mtu hatari kwenye matumizi ya aina yoyote ya silaha.

Vile vite alitaarifiwa kwamba ninajua sarakasi sana na wakati nilipokuwa Japan niliwahi kushindana na bingwa Inoki na kutoka naye sare. Watu wanashangaa kwa nini sikuendelea kwani bila shaka sasa ningalikuwa bingwa wa dunia.

Jibu maswali kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maeleo. Si lazima kuandika sentensi kamili.

- (a) Mwandishi anaelezeaje mandhari?

(1)

- (b) Willy Gamba amefanya nini ili kuingia chumbani?

Toa maeleo **mawili**

(2)

- (c) Tunajuaje kwamba Veronika amemkasirikia Willy Gamba?

Toa maeleo **mawili**.

(2)



(d) Taja sababu ya hasira za Veronika

(1)

(e) Willy Gamba ana elimu gani?

Toa maelezo **mawili**.

(2)

(f) Tunajuaje kwamba Willy Gamba ana ujuzi mkubwa wa sarakasi?

Toa maelezo **mawili**

(2)

(Total for Question 4 = 10 marks)

TOTAL FOR SECTION A = 38 MARKS



P 7 1 0 7 7 A 0 9 1 6

SECTION B**Writing**

Answer Questions 5 and either Question 6(a) or 6(b) or 6(c).

Write your answers in the spaces provided.

5

Vyakula vyakula kukaangwa

Vyakula ulivyofurahia
awali

Vyakula kwa afya
bora

Vyakula
utakavyopendelea

Ushauri

Andika takriban maneno 70 kwa **Kiswahili** kuhusu vyakula vyakula kukaangwa. Ni lazima kutumia maneno yote yaliyotajwa hapo juu.

(12)



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

(Total for Question 5 = 12 marks)



P 7 1 0 7 7 A 0 1 1 1 6

- 6 Chagua **moja** kati ya maswali matatu yafuatayo na andika takriban maneno 130 kwa **Kiswahili**.

Chaguo 1

(a)



Andika makala kuhusu matumizi ya teknolojia. Ni lazima uandike kuhusu:

- Umuhimu wa teknolojia kwa wakati wa sasa
- Uzoefu wako wa kutumia teknolojia
- Teknolojia itakavyokuwa na athari baadaye

(20)

Chaguo 2

(b)

Mpendwa Hannah

Nimemaliza mithiani yangu yote na sasa ninawaza kuhusu mwaka ujao. Sijaamua ajira nitakayopenda kufanya, vipi wewe?

Rafikiyo,

Aaliyah

Jibu kwa kutumia barua pepe. Ni lazima uandike kuhusu:

- Mipango yako kwa mwaka ujao
- Uzoefu wako kuhusu ajira iliyopita
- Maoni ya Hannah kuhusu kazi bora zaidi

(20)

Chaguo 3

- (c) Kwenye ukurasa wako wa blogu andika kuhusu mambo unayopenda kufanya. Ni lazima uandike kuhusu:

- Maelezo ya shughuli uipendayo
- Umefanikiwa kupata nini kutokana na shughuli uipendayo
- Mawazo yako kuhusu kufanya shughuli uipendayo kuwa ajira

(20)



Indicate which question you are answering by marking a cross in the box . If you change your mind, put a line through the box and then indicate your new question with a cross .

Chosen question number: **Question 6(a)** **Question 6(b)**
Question 6(c)



P 7 1 0 7 7 A 0 1 3 1 6

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

(Total for Question 6 = 20 marks)

TOTAL FOR SECTION B = 32 MARKS



P 7 1 0 7 7 A 0 1 4 1 6



SECTION C**Translation into Swahili****Write your answer in the space provided.**

- 7 Tafsiri aya ifuatayo kwa **Kiswahili**.

Saving Rhinos And Elephants From Poachers

Kerry, who grew up on a farm, has always been passionate about wildlife. It was on a research trip to Africa that she realised how much she cared for them. Once on location she found out that a huge number of women were joining the fight against poaching. This traditionally male-dominated battle is very important for animal welfare. Most women take various jobs from being guards to veterinarians and lawyers.

Kerry says, "when women say they're trailblazers, it is correct. When I got off the plane, I was exhausted but they just worked."

(Total for Question 7 = 10 marks)

TOTAL FOR SECTION C = 10 MARKS**TOTAL FOR PAPER = 80 MARKS**

P 7 1 0 7 7 A 0 1 5 1 6

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

BLANK PAGE

Source information

Question 2

- © mimagephotography/Shutterstock
- © fizkes/Shutterstock
- © Jasminko Ibrakovic/Shutterstock

Question 6

- © Flamingo Images/Shutterstock

